# Together

## Kusanyiko la Watu wa Mungu

# Vifaa vya vyombo vya habari

## Tangazo la Papa Francisko

Siku ya Jumapili tarehe 15 Januari 2023, baada ya sala ya Malaika wa Bwana kwenye Uwanja wa Mtakatifu Petro, Baba Mtakatifu alisema:

> *"Njia ya umoja wa Kikristo na njia ya wongofu wa Sinodi ya Kanisa imeunganishwa* pamoja*. Napenda kuchukua fursa hii kusema kwamba Jumamosi tarehe 30 Septemba, mkesha wa maombi ya kiekumene utafanyika kwenye Uwanja wa Mtakatifu Petro ambapo tutamkabidhi Mungu kazi ya Mkutano Mkuu wa 16 wa kawaida wa Sinodi ya Maaskofu. Kwa vijana wanaokuja kwenye mkesha huu, kutakuwa na programu maalum katika wikendi hiyo yote, itakayoongozwa na jumuiya ya Taizé. Kuanzia sasa na kuendelea, ninawaaalika kaka na dada wa madhehebu yote ya Kikristo ili kushiriki  maombi katika "Kusanyiko hili la Watu wa Mungu."“*

## Mradi wa "Pamoja" kwa ufupi

Vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 kutoka nchi mbalimbali za Ulaya na kutoka madhehebu yote ya Kikristo wanaalikwa kuja mjini Roma kuanzia Ijumaa jioni hadi Jumapili alasiri kwa wikendi ya ushirika. Watakaribishwa kwenye parokia na jumuiya zilizo kwenye mji mkuu wa Roma na kukaa na wenyeji. Kwa vijana Wakatoliki, tukio hili linaweza kutekelezwa kama ufuatiliaji wa Siku ya Vijana Duniani ambayo itafanyika Lisbon mwanzoni mwa mwezi wa Agosti.

Kiini cha wikendi hii ya ushirika ni mkesha wa maombi ya kiekumene huko mjini Roma tarehe 30 Septemba 2023, pamoja na Baba Mtakatifu Francisko na wawakilishi wa makanisa mbalimbali. Maombi haya, ambayo yatakuwa wazi kwa watu wote wa Mungu, yatajumuisha kusikiliza Neno la Mungu, sifa na maombezi, nyimbo za Taizé na ukimya – kielelezo kikubwa cha ushirikiano, umoja na amani.

## Uhusiano na Sinodi ya Kanisa Katoliki

Mkesha wa maombi ya kiekumene utafanyika katika mkesha wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Kawaida wa Sinodi ya Maaskofu, utakaokuwa na mada yake: "Kwa ajili ya Kanisa la Kisinodi: Umoja, Ushiriki na Utume." Sinodi hii itafanyika kuanzia tarehe 4 hadi 29 Oktoba 2023. Kama alivyosema Baba Mtakatifu Francisko katika tangazo lake la tarehe 15 Januari 2023, mkesha huu ni sehemu ya safari ya kisinodi na ya kiekumene: “Njia ya umoja wa Wakristo na ile ya uongofu wa Sinodi ya Kanisa zinaambatana."

Zaidi ya hayo, Papa Francisko tayari alikuwa ameshasisitiza uhusiano wa karibu ulio kati ya usinodi na uekumene, wakati wa hadhara yake na Mtakatifu Mar Awa III (tarehe 19 Novemba 2022) pale alipothibitisha ya kwamba "kama jinsi njia ya kiekumene ilivyo ya kisinodi vile vile njia ya kisinodi (...) ni lazima iwe ya kiekumene". Kwa hiyo, uwepo wa viongozi wa Makanisa mbalimbali ya Kikristo kwa ajili ya mkesha huo wa maombi ya kiekumene huko mjini Roma, na katika mkesha wa kusanyiko la sinodi, utakuwa na umuhimu usio na kifani.

## Mwanzo wa mradi

Mnamo Oktoba 2021, Bruda Alois, mkuu wa jumuiya ya Taizé, alialikwa kuzungumza katika ufunguzi wa Sinodi ya Maaskofu kuhusu usinodi huko mjini Roma. Miongoni mwa mambo aliyosema alipohutubia washiriki, ni kwamba:

> *“Ninaonelea ya kwamba ingekuwa bora kuwe na nyakati za kuweza kupumua katika safari ya kisinodi, kwa mfano, kusimama na kusherehekea umoja ambao tayari umepatikana katika Kristo na kuufanya udhihirike. (...) Je, itawezekana siku moja, katika hatua za mchakato wa kisinodi, si wajumbe tu bali watu wote wa Mungu, si Wakatoliki pekee bali waumini kutoka katika Makanisa mbalimbali kualikwa kwenye kusanyiko kubwa la kiekumene? Kwa maana kwa njia ya ubatizo na Maandiko, je, sisi si ndugu katika Kristo, waliounganishwa katika ushirika ambao bado haujakamilika, lakini ambao ni wa kweli, hata wakati maswali ya kitheolojia yanapobaki bila kujibiwa. (…) Tungegundua ya kwamba kwa kuunganishwa katika Kristo, tunaweza kuwa wapatanishi.*

## Maana ya kusanyiko lenyewe

Ndani ya mfumo wa mchakato wa sinodi ya Kanisa Katoliki, “Kusanyiko hili la Watu wa Mungu” linalenga kuonyesha nia ya kudhihirisha wazi zaidi umoja wa Wakristo “wasafirio”. Hapa kuna nukuu kutoka kwa uwasilishaji wa mradi uliochapishwa kwenye wavuti www.together2023.net:

> *“Je, si Kristo anayetuita na kutufungulia njia ya kusonga mbele pamoja naye kama wasafiri wenziwe, pamoja na wale wanaoishi pembezoni mwa jumuiya zetu? Katika safari hii, katika mazungumzo yanayopatanisha, tunataka kukumbuka ya kwamba tunahitajiana, si ili tuwe na nguvu pale tunapokuwa pamoja bali kuchangia kwenye amani katika familia ya binadamu. Katika kushukuru kwa hisia hii inayokua ya ushirika, tunaweza kupata motisha unaohitajika ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazotukabili pamoja na migawanyiko inayoivunja familia ya binadamu na kilio cha dunia. Katika kukutana na kusikilizana, na tutembee pamoja kama watu wa Mungu.”*

# Maswali ya vitendo

## Lini?

Kuanzia Ijumaa, tarehe 29 Septemba hadi Jumapili tarehe 1 Oktoba 2023.

## Wapi?

Kwenye Mji mkuu wa Roma na sehemu mbalimbali duniani.

## Nani anahusika katika maandalizi?

Tayari makundi hamsini ya asili zote za madhehebu ya makanisa,: Makanisa na mashirikisho ya kikanisa, jumuiya na makundi ya kikanisa, huduma ya vijana. Kwa mpango wa Taizé na kwa ushirikiano wa karibu na Sekretarieti ya Sinodi ya Roma, *Dicastery* ya Kukuza Umoja wa Wakristo, *Dicastery* kwa Walei, Familia na Maisha, na *Vicariate*. Orodha ya washirika wanaohusika itasasishwa mara kwa mara kwenye tovuti ya tukio: www.together2023.net .

## Nani anahusika katika maandalizi?

Mkesha wa maombi ya Jumamosi uko wazi kwa kila mtu. Vijana kutoka umri wa miaka 18 hadi 35 wanaweza kuja mjini Roma kutoka Ijumaa jioni hadi Jumapili. Watakuwa wenyeji wa parokia na jumuiya za Kikristo za jiji hili.

## Je, itakuwa mpango gani kwa vijana?

### ✗ Kuwasili siku ya Ijumaa

Vijana wanaoshiriki wikendi nzima wanapaswa kuwasili Ijumaa alasiri tarehe 29 Septemba. Watapangiwa parokia itakayowakaribisha.

### ✗ Jumamosi asubuhi

Jumamosi asubuhi tarehe 30 Septemba itaanza na programu iliyogawanywa katika "njia" tofauti na mikutano katika sehemu tofauti za mji mkuu wa Roma.

### ✗ Warsha & “baraza/majadiliano”

Washiriki watashiriki katika warsha na “baraza/majadiliano” juu ya mada tofauti katika makanisa ya madhehebu tofauti na za sehemu nyingine.

### ✗ Sifa na Ibada

Kivutio kikuu cha wikendi kwa vijana kitakuwa wakati wa kusifu na kuabudu katika eneo la kipekee katikati mwa Roma mwanzoni mwa alasiri siku ya Jumamosi.

- ✗ Mkesha wa maombi

Mkesha huu wa maombi ya kiekumene uliofunguliwa kwa kila mtu utafanyika kwenye Uwanja wa Mtakatifu Petro mjini Roma siku ya Jumamosi jioni. Papa Francisko na wawakilishi wa Makanisa mbalimbali watashiriki.

## Nembo

Mchoro wa hema unakumbusha mstari katika Kitabu cha Isaya 54:2: “Panua nafasi ya hema yako!” Pia ni mwaliko wa kuja pamoja "kwenye hema moja".

Mchoro wa watu- unaelezea ubinadamu wetu katika anuwai zote za hali ya maisha, vizazi na asili. Unaonyesha watu wa Mungu wakiwa njiani kuelekea kwenye hema, nafasi ya ushirika na mahali pa uwepo wa Mungu.

## Kushiriki katika maandalizi

Vikundi kumi vya utendakazi vinaundwa ili kufuatilia vipengele na changamoto mbalimbali za maandalizi. Usajili wa vikundi hivi bado unawezekana kwa kuwasiliana na volunteers@together2023.net .

## Je, ni hatua gani zinazofuata?

- Kuanzia tarehe 12 hadi 15 Machi 2023: mkutano huko mjini Roma wa wajumbe kutoka kwa vikundi mbalimbali vya makanisa yanayohusika, na uwezekano wa kushiriki mtandaoni.
- Mwishoni mwa mwezi wa Machi hadi katikati mwa mwezi wa Juni 2023: timu ya wafanyakazi wa kujitolea itakuwa ikifanya kazi kwenye tovuti huko mjini Roma kutembelea parokia na jumuiya za Kikristo na kukabiliana na changamoto mbalimbali za ugavi na usafirishaji wa watu.

## Kwa maelezo zaidi

- Tovuti rasmi ya tukio: **www.together2023.net**
- Facebook / Instagram: : **@30Sept2023 | #Together2023**
- Twitter: **@Together2023**

## Bonyeza anwani

media@together2023.net